

**MOJAWAPO YA MTIHANI MGUMU NA**  
**AMBAO WANAFUNZI WA YESU KRISTO**  
**HAWAUPENDI NDIYO HUU**

**MAANDIKO: MATH 5:10-12, 43-48**

**1. UTANGULIZI:**

Kufurahi pamoja na kushangilia wakati **umeudhiwa** na **kushutumiwa** na **kuzushiwa** jambo ambalo hujalitenda bali ni uongo ni mtihani unaohitaji Neema ya Mungu kukusaidia, maana kawaida ya moyo wa binadamu pindi anaposhutumiwa na kuzushiwa na kunenewa maneno makali kwa uongo moyo wake huwa unajeruhiwa /unaumizwa! Bali Yesu anasema mtihani huu ndiyo ulio na thawabu (Reward) mteule akiushinda na Ufalme wa Mbinguni unakuwa wake na anakuwa amekamilika kama Mungu Baba wa Mbinguni alivyo mkamilifu!!

- Katika Ulimwengu huu, unapookoka na kuamua kutetea viwango vya Mungu vya kweli, Utakatifu haki pamoja na kuishi maisha ya usafi pasipo kujichafua, na kukataa kata kata kufanya suluhu na uovu, lazima ulimwengu **utakuchukia, utakupinga, utakuudhi, utakushtumu n.k Math 10:22, 24:9 na Yoh 15:18-19**, kipindi kama hiki ndicho Yesu anasema ufurahi na kushangalia maana thawabu yako ndipo inapoandaliwa!! na **Mtume Paulo alienda mbali zaidi; 2Timoth 2:11-12**

2. Kanuni za Ufalme wa Mungu kamwe hazibadiliki yaani woote wapendao kuishi maisha ya utaua katika Kristo Yesu lazima tu wapitie **maudhi, mashutumu, kunenewa uongo!! 2Timoth 3:12** ni katika kipindi kama hiki

ambacho Mungu anaupima upendo wetu kwa wale wanaotuudhi na kutushutumu kama tunawaombea na wakati huo huo kuvumilia mateso yote kwa sababu ya kulinda Imani yetu na Yesu Kristo. **Huu siyo mtihani rahisi, siyo mtihani wa kuchagua jibu hata kwa kubahatisha tu ukapata!! Ni mtihani unaohitaji kukaa chini na kumtafakari sana Yesu Kristo kwamba yeye alifanyaje pindi aliposhutumiwa na kuudhiwa na kunenewa maneno mengi ya uongo!! Ebr 12:1-3, Luk 23:32 -38**

- Yesu alifundisha wanafunzi wake somo hili na yeye mwenyewe akapitia katika mtihani huu mgumu sana na alipofurahi na kuwapenda adui zake waliomtenda mabaya na kumshutumu ndipo Baba akampa thawabu kubwa ipitayo thawabu zote kulingana na kiwango cha maudhi aliyopata na mashutumu na kuaibishwa kwa kiwango cha hali ya juu kuliko binadamu yeyote au Nabii aliyemtangulia na atakayekuja baadae. **Filp 2:9-11, Mdo 4:12.**
  - **Baba yetu wa Imani Ibrahimu** naye alishinda mtihani huu pale Lutu alipoanzisha ugomvi na yeye pamoja na Wachungaji wake baada ya kufanikiwa na kuwa na mali kama yeye- **Mwanz 12:1- 4, 13:1- 18, 14:8 - 20, 16:-33, 19:1-24.**
  - **Yusufu** alishinda mtihani huu naye- **Mwz. 37: 15 – 28, Mwanz 45:1-15, 50:14-21.**
3. Kuwapenda na kuwaombea wale wote wanaotuudhi na kutushutumu kwa sababu tumekataa njia ya walimwengu bali kuishi maisha ya usafi na utaua, na kisha kufurahi na kushangilia katika kipindi hicho ndiyo njia pekee inayoondoa uchungu wote ndani ya moyo na kukufanya utembe ukiwa mwepesi, bila kuwa na mzigo wowote mzito wa watu moyoni mwako na hivyo kumpendeza Mungu Baba anayewanyeshea mvua watu wema na waovu!! **Math 5:45**

- Nakama kuna eneo adui shetani anafaulu sana ni hili la kujeruhi moyo wa mteule kwanza kwa maneno makali pamoja na shutuma nyingi zisizo na sababu ili ajaze uchungu moyoni mwake (majeraha) jambo ambalo litampelekea ashindwe kuomba, ashindwe kulala usingizi, apande **B.P** na hivyo kuwa rahisi kuendeshwa na ibilisi kama anavyotaka.
- **Mizigo ya watu wanaotujeruhi na kutuumiza ikibebwa ndani ya moyo ni mizito mno kuliko hata mizigo tunayobeba vichwani au mabegani na kamwe kwa sababu ya uzito wake, itatuchosha, itatuzeesha haraka, itatunyima thawabu mbele za Mungu na kwa vyovyote vile Mbinguni hatutaingia. Zab. 51:10-11 na Ezek.11:17-20.**
- Ni hatari kama mwana wa Mungu kuishi pamoja na kutembea ukiwa na moyo uliobeba watu, uliojeruhiwa; **majeraha ya nje ya mwili yakiwepo watu huyashughulikia kwa gharama zozote ili yapone maana wanajua madhara yatakayotokana na majeraha hayo!!** Si zaidi sana majeraha ya ndani ya moyo ambayo hayaonekani kwa macho haya ya nyama, yasiposhughulikiwa leo na mwana wa Mungu akatoka katika ibada hii ameyatunza tu moyoni mwake kwa vyovyote vile kesho yatazalisha uchungu usioisha na baada ya muda siyo mrefu mteule atakufa Kiroho kabisa na thawabu yake Mbinguni inafutwa na mwishowe anasafiri kwa uzito na anamaliza safari yake vibaya. Kila mmoja wetu hapo alipo anao mtihani huu mgumu ambao lazima aifanye!! **2Timoth 3:12** Mungu atupe uelewa wa ndani Kiroho juu ya mtihani huu. **Na laiti kila mmoja wetu angejua kwa kina madhara ya kutembea na moyo uliojaa majeraha na uchungu. Ebr. 12:14-15. Amen**

**Na**

**Ask Dr L. M Mwizarubi**

**June 2021**